



REPUBLIC OF KENYA

**HOTUBA YA MHE. REBECCA MIANO, EGH, WAZIRI,
WIZARA YA UWEKEZAJI, BIASHARA NA VIWANDA,
KATIKA MAKABIDHI WA MICHANGO KWA
WAATHIRIKA WA MAFURIKO KATIKA KAUNTI
NDOGO YA DAGORETTI KUSINI, TAREHE 8 MEI, 2024**

SALAMU

- Mbunge wa Eneo hili,
- Katibu Mkuu
- Utawala wa Serikali ya Kitaifa
- Mabibi na mabwana

**1. Ndugu Wakazi wa Kituo cha Dagoretti South muliofika
hapa Mutuini Primary School, Hamjambo? MUNGU NI
MWEMA.. NA KILA WAKATI?**

**2. Kwanza ninawashukuru kwa makaribisho yenu leo hii,
na ninawaletea salamu kutoka kwa Rais wetu, Mhe.
William Samoei Ruto.**

3. Leo hii, nimekuja kuwa nanyi na kuwapa pole mlioathirika na msimu huu wa mvua kubwa inayoendelea kunyesha.
4. Kwa kweli, mvua hii inayosababishwa na kubadilika kwa tabianchi imeleta mafuriko yaliyoleta uharibifu mkubwa. Nimesikia waliozungumza hapa wakituambia tabu walizopata; imeharibu nyumba zenu, sehemu munazoishi, na hata biashara zenu. Poleni sana
5. Hata hivyo, nimefurahi kuona kuwa hamjavunjika moyo. Ninaona nyuso zilizo na furaha. Hasa kina Mama! Ninawapa pongezi kwa ujasiri na ushirikiano wenu hata katika kipindi hiki kigumu. KINA MAMA OYEEE! NA VIJANA NANYI OYEE!
6. Serikali yetu, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais William Ruto, imeweka mpango kabambe ya kuhamisha wananchi kutoka sehemu zilizoathirika na pia kutoa misaada kwa wale walioathiriwa na janga hili. Ningeomba sote tushirikiane na mamlaka tuhamie kwa maeneo yaliyo salama.

7. Katika Wizara yangu, tumejitolea kutoa msaada munaohitaji. Hivyo basi, nimekuja na wanzangu na nataka niwajulishe viongozi walio hapa na mimi.

(INTRODUCE STAFF)

8. Sote tumekuja kuungana nanyi na kuwahakikishia kuwa tuko pamoja nanyi.

9. Wafanya kazi wote kutoka Makao Makuu ya Wizara yangu, Idara za Uwekezaji, Biashara na Viwanda, na Mashirika yaliyo chini ya Wizara yangu wamejitolea na kuchanga ili kuwaletea vyakula na bidhaa munazohitaji:

10. Baadhi ya vitu tulivyowaletea ni:

i. **Vyakula**, kama Unga wa mahindi na wa ngano, mchele, mafuta ya kupikia, maji ya kunywa.

ii. **Pia bidhaa munazohitaji:** Blanketi, Godoro, ndoo, sabuni, na pedi za usafi za wanawake

11. Ninakabidhi bidhaa hizi kwa mbunge wenu na timu yake ili waweze kuwagawanyia wakihakikisha kuwa kila mtu aliyehapa amepata usaidizi huu.

12. Nikimalizia, natoa wito kwa mashirika ya maendeleo na wafadhili kutoka sekta binafsi na jamii tuungane pamoja ili tuwasidie wakenya wenzetu—Kutoa ni moyo. Tuzingatie maslahi ya wengine na kuwasaidia wenye uhitaji.

Asante,

Mungu awabariki.